

## **SURA YA SITA.**

### **“Mwisho sio wakati.”**

Maisha ni stori za tafsida na tawira, kwangu Maisha ni fasihi licha ya kuniburidisha na kunielimisha, nisijibie nafsi yako katika hili. Nashukuru kutenga muda wako wa thamani kusoma Riwaya ya Jicho. Kama itakupendeza nipatie Jicho lako lenye maudhui uliyoyapata tucheze.

“Mchezo wa fasihi. Kila mwanzo una mwisho ila mwisho ni hatua ya mabadiliko tofauti na awali. karibu kwenye mchezo”

“Kila kitendo kinachoumba ni cha pekee kitendo kinachoharibu”. fikiri kuhusu jicho na ubongo lipi ni muelekeo bora? Fikiri kuhusu uhuru, sio wa taifa au serikali lakini wa kwako? Fikiri kuhusu muda na ratiba yako? Fikiri uhusiano wa shule na ajira? Fikiri kuhusu mwenye haki ya chuki ingali maadili yameficha haki yake? Nachukia neno mwisho sababu hakuna mwenye uzoefu na nyakati hizo. Naamini kioo ni Rafiki wa kweli wa Jicho nililolidhamiria.

# AMANI NI TIBA ILYOSALIA KWA WALIO HAI



**An eye for an eye will only make the whole world blind  
-MOHANDAS GANDHI**